

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA  
Nambari ya Simu: +255 026 – 2323267  
E- Mail Na. [ps@afya.go.tz](mailto:ps@afya.go.tz)



Mji wa Serikali Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S.L. P 743,  
40478 DODOMA.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**WADAU WAENDELEA KUUNGA MKONO MAPAMBANO DHIDI YA CORONA NCHINI**

**Dar es Salaam, Jumamosi Aprili 18, 2020**

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Ummu Mwalimu kwa niaba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa amepokea misaada mbalimbali yenye jumla ya **Shilingi bilioni 3.2** kutoka kwa wadau mbalimbali, makampuni binafsi na wadau wa maendeleo katika kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona (COVID-19) hapa nchini.

Sehemu ya misaada hiyo iliyokabidhiwa na kupokelewa na Waziri Ummu ni fedha zilizowasilishwa kwa mifano ya **hundi zenye jumla ya Shilingi 3,185,500,000.00** na **vifaa kinga na tiba** vilivyotolewa na Taasisi ya Lotary Club ya Bahari jijini Dar es Salaam **vyenye thamani ya Shilingi 15,000,000.00** kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za Serikali za kukabiliana na ugonjwa wa Corona (COVID-19).

Akipokea misaada hiyo Waziri Ummu amesema misaada hiyo itaelekezwa zaidi na Serikali katika kuongeza na kununua zaidi vifaa kinga kwa ajili ya wataalamu wa afya ambao wako mstari wa mbele katika kutoa huduma kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwezesha utoaji wa mafunzo zaidi kwa wataalamu wetu ambao wanapambana usiku na mchana ili kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wahisiwa na wagonjwa wa Corona (COVID-19).

Taasisi na kampuni ambazo zimetoa msaada ya fedha kwa mfano wa hundi ni pamoja na: Kampuni ya SAN & LAM (Tzs.172,500,000.00), FAIDA-Letshego Bank (Tzs.33,000,000.00), Financial Sector Depending Trust-FSDT (Tzs.225,000,000.00), TUICO TAIFA (Tzs.10,000,000.00), Kampuni ya Huduma za Simu - VODACOM (Tzs.2,300,000,000.00), Kampuni ya SONGAS (Tzs.100,000,000.00), Kampuni ya YEPI MARKEDZI (Tzs.200,000,000.00), Benki ya NBC (Tzs.80,000,000.00), na Shirika la Reli Tanzania – TRC (Tzs.65,000,000.00).

Ikumbukwe kuwa mpaka kufikia jana Aprili 17, 2020 kwa taarifa rasmi iliyotolewa na Waziri Ummu, Tanzania ina jumla ya jumla ya watu **147** waliopata maambukizi ya virusi vya Corona (COVID – 19) nchini huku kati ya hao waliopona wakiwa ni **11** na vifo **5** vilivyothibitishwa tangu kuanza kuripotiwa kwa ugonjwa huu hapa nchini tarehe 16 Machi 2020. Hili ni ongezeko la wagonjwa wapya 53 wenye maambukizi ya virusi vya Corona kutoka wagojwa 94 na kifo kimoja (1) alivyovitolea taarifa za awali.

*Pamoja na hilo Waziri Ummu ametangaza maamuzi ya Serikali kuamua kutumia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana (Dar es Salaam) kama Kituo Maalum cha Matibabu ya Ugonjwa wa CODIV-19 na kuwataka wananchi wa Dar es Salaam wanaohitaji kupata huduma za matibabu ya magonjwa mengine katika Hospitali ya Amana kutumia hospitali nyingine zilizopo mkoani hapa.*

**Kwa uzito wa pekee Waziri Ummu ametoa wito kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuendeleza jitihada hizi za Serikali katika kuwabaini na kuwashughulikia watu wote wasio na nia njema na Serikali na Taifa kwa ujumla kwa kuendelea kusambaza taarifa zisizo rasmi na zisizo na ukweli kwa jamii na hivyo kusababisha taharuki kubwa za mara kwa mara na wakibainika wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi.**

Wizara inapenda kuwakumbusha tena wananchi kuendelea kuzingatia na kufuatilia maelekezo ya wataalam wa afya katika kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka, kuepuka misongamano na kukaa umbali wa zaidi ya mita moja baina ya mtu na mtu na wananchi wenye dalili za ugonjwa wa Corona (COVID-19) wanashauriwa kuwahi hospitali kupata ushauri na huduma ya afya na kujitenga ili kuepuka kusambaza maambukizi kwa wengine.



Gerard Julius Chami

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali  
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO - AFYA**